



OFISI YA RAIS TAMISEMI HALMASHAURI YA MJI KONDOA JARIDA LA HALMASHAURI



Oktoba— Desemba 2020

Mhe. Jafo aipa Kongole Halmashauri ya Mji Kondoa



Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Seleman Jafo (wa kwanza kushoto) Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Dkt. Suleman (katikati) na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa wakiwasili katika Shule ya Sekondari Ula wakati wa ziara ya Mhe. Jafo shuleni hapo hivi karibuni

SERA YA UHARIRI

Madhumuni ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Mji Kondoa. Aidha Sera, Mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kupitia jarida hili. Isipokuwa pale inapokatazwa habari za Jarida la Halmashauri ya Mji Kondoa zinaweza kunukuliwa ili mradi Mhariri ajulishwe kwa maandishi.

NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI



Msoleni Dakawa

Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondo

Bodi ya Uhariri

Msoleni Dakawa

Sekela Mwasubila

Flora Kyaruzi

Mawasiliano

S.L.P 711 Kondo

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255262360313

Mitandao ya Kijamii



[www: kondoatc.go.tz](http://www.kondoatc.go.tz)



Kondo TC



kondoatc2015



KondoTC



@KondoTC

Barua Pepe
td@kondoatc.go.tz

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha hadi siku ya leo na kumaliza salama utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba—Desemba) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Pili nampongeza Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa tena kuiongoza nchi kwa kipindi cha miaka mitano tena sambamba na waheshimiwa madiwani katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, 2020 nawakaribisha tufanye kazi kwa pamoja ya kuwahudumia wananchi.

Tatu katika kipindi hicho Halmashauri ilisimamia ufanyaji wa mitihani wa darasa la VII, 2020 ambapo jumla ya wanafunzi 1489 walifanya mitihani hiyo. Pia mtihani wa upimaji taifa darasa la nne uliofanyika ambapo jumla ya wanafunzi 2210 walifanya mtihani huo.

Nne Halmashauri kwa upande wa Elimu Sekondari kwa kipindi hicho imesimamia zoezi la ufanyaji wa mtihani wa kumaliza kidato cha pili ambapo jumla ya wanafunzi 857 walifanya mtihani halikadhalika wanafunzi 1197 wa kidato cha pili walifanya mtihani wa kitaifa kwa kidato cha pili.

Aidha katika kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba 2020 Halmashauri ya Mji imepokea fedha kiasi cha Shilingi 183,317,680.55 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Mfuko wa jimbo Tshs. 27,022,000, Elimu bila Malipo Tshs. 142,839,417.55, EGPAF Tshs. 11,382,723, GLOBAL FUND Tshs. 1,073,540 na mradi wa Malaria Tshs. 1,000,000) na kuifanya Halmashauri kupokea asilimia 5.6 ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Hata hivyo kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba Halmashauri kupitia mapato ya ndani imekusanya shilingi milioni 704,514,500.51 sawa na asilimia 50 ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2020/2021 na kutenga shilingi milioni 33,141,000 ikiwa ni asilimia kumi ya makusanyo kwa ajili ya mikopo ya Vijana, Wanawake na watu wenye ulemavu.

Mwisho niwaombe wananchi wa Halmashauri ya Mji Kondo kuendelea kuwapeleka watoto wao waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kufika shuleni na kuanza masomo na serikali itawachukulia hatua wazazi wote ambao hawatawapeleka watoto wao kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2021.

BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI 2020-2025



Mhe. Mohamed Kiberenge
Mwenyekiti wa Halmashauri




Mhe. Juma Makoa
Mbunge Kondoza Mjini




Mhe. Besela Maunga
M/Mwenyekiti wa Halmashauri



Mhe. Ramla Abeid
Diwani kata ya Bolisa



Mhe. Issa Kambi
Diwani Kata ya Kilimani




Mhe. Japhari Ganga
Diwani Kata ya Suruke



Mhe. Fatuma Idd
Diwani V/M Kondoza Mjini



Mhe. Kulwa Pazi
Diwani Kata ya Serya



Mhe. Abushehe Mbuva
Diwani Kata ya Kingale



Mhe. Zainab Haroub
Diwani Kata ya Chemchem



Mhe. Rachel Sombida
Diwani V/M



Mhe. Idd Ng'ungu
Diwani Kata ya Kolo

Mhe. Jafo aipa Kongole Halmashauri ya Mji Kondo

Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Seleman Jafo amewapongeza viongozi na watumishi wa Halmashauri ya Mji Kondo kwa kusimamia vizuri miradi ya ujenzi wa madarasa na kuwataka kuongeza juhudi katika kufanya kazi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma.

Ameyasema hayo wakati wa ziara yake ndani ya Halmashauri ya Mji Kondo katika ukaguzi wa miradi na kuongea na watumishi akiongozana na wataalam kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

“Kabla ya kuja hapa nilipita katika miradi nimekagua jengo jipya la Halmashauri jengo ni zuri hongereni linaendana na nyie ila lipo nyuma ya muda sijaridhika ikifika Februari 1 nataka Mkurugenzi na watumishi wako mhamie kule lakini miradi ya ujenzi wa madarasa ipo vizuri ila wakati mwingine mzingatie ushauri nilioutoa ili tuwe na majengo yatakayodumu kwa muda mrefu,”amesema Mhe. Jafo

Aidha amewashauri kuongeza mapato kwa kubuni vyanzo vipya ambavyo havitawaumiza

wananchi ili kupata fedha ni kazi kwa kupendana



Waziri wa OR TAMISEMI Mhe. Seleman Jafo akiwa katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Msingi Maji ya Shamba baada ya kukagua madarasa yanoonekana pichani.

za kutosha kwa ajili ya kuiendesha Halmashauri na kuondokana na utegemezi wa serikali japokuwa wanafanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato.

“Watumishi wote fanyeni



Watumishi wa Halmashauri ya Mji Kondo wakimsikiliza Waziri wa OR TAMISEMI Mhe. Seleman Jafo (hayupo pichani) alipofanya ziara hivi karibuni

kwa kujituma zaidi na hemu ya marejesho zitu- mnapopewa kazi zifanyeni mike kwaajili ya ufuatiliaji kwa wakati ila kubwa fanye- wa mikopo hiyo.

kwani muda mwingi watumishi mnautumia mkiwa kazini katika baadhi ya maeneo watumishi wa idara moja hawaongei hii inapunguza pia utendajikazi kwani wanaopendana

hufanyakazi vi- zuri,”amesisitiza Mhe. Jafo Aidha amewataka watumishi Idara ya Maendeleo ya Jamii kusimamia asilimia kumi za mapato na

kuhakikisha zinawafikia walengwa kwani katika baadhi ya maeneo fedha hizo zimekuwa hazitolewi kuto- kana na waku- rugenzi kuzuia fedha hizo

kutoka na kuahidi kusimamia mapi- tio ya kanuni za mikopo hiyo ili se-

wa mikopo hiyo.

Mhe. Jafo aipa Kongole Halmashauri ya Mji Kondo



Waziri wa Nchi OR TAMISEMI Mhe. Seleman Jafo akiongea na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ula baada ya kukagua madarasa yanoonekana pichani.

Inatoka Uk. 4...

Akiongea awali Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Suleman Serea amemshukuru Mhe. Waziri kwa ziara yake ndani ya mkoa wa Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa miradi ambapo serikali imetoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi na kumuahidi kusimamia maagizo yote yaliyotolewa ili kuhakikisha huduma inatolewa kwa wananchi.

Akimkaribisha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondo Mkurugenzi Msoleni Dakawa amesema katika mwaka wa fedha 2017/18 halmashauri

ilikisia kukusanya shilingi milioni 800 lakini mpaka kufika mwisho wa mwaka wa fedha ilikusanya shilingi bilioni 1.2 sawa na 133% na mwaka 2018/19 ilikisia kukusanya shilingi bilioni 1.6 mara mbili zaidi ya mwaka ulioisha na hadi kufikia 30 Juni 2019 Halmashauri ilikusanya shilingi 1.4 sawa na 88% hata hivyo kutokana na changamoto mbalimbali katika mwaka wa fedha 2020/21 imekisia kukusanya shilingi bilioni 1.4 na inaendelea kubuni vyanzo vingine vya mapato ili kukusanya mapato mengi zaidi bila kumuathiri mwananchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondo

Mhe. Mohamed Kiberenge amemshukuru Mhe. Waziri kwa kumatembelea na kumuahidi kufanya kazi kwa kushirikiana na Mkurugenzi na watumishi wote ambao ana imani kubwa nao kutokana na utendaji wao mzuri kwa lengo la kuibadilisha Halmashauri ya Mji Kondo.

Ziara ya Mhe. Jafo imefanyika ikiwa ni mwendelezo wake wa kutembelea Halmashauri na kukagua miradi ambapo alipata fursa ya kutembelea ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Mji Kondo lililoghaliwa zaidi ya shilingi bilioni 3, ujenzi wa madarasa shule ya Msingi Maji ya Shamba na Shule ya Sekondari Ula ikiwa ni kati ya shule 7 zilizopokea shilingi milioni 291

"Madaktari kuweni waaminifu kupinga ukatili wa kijinsia"- Mkurugenzi Dakawa



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa akitoa neno wakati wa kuadhimisha kilele cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia katika ukumbi wa Kondoa Irangi

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa amewataka baadhi ya madaktari kuwa waaminifu kwa kuandika ripoti zenye uhalisia ili haki itendeke kwa wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia.

Ameyasema hayo wakati akifungua mdahalo wa kuadhimisha kilele cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia uliofanyika katika ukumbi wa Kondoa Irangi hivi karibuni.

"Kesi nyingi zinakosa ushahidi sababu tu daktari kaandika ripoti yenye kupindisha ukweli kuhusu uchunguzi wake na mwisho wa siku ikienda mahakamani mtuhumiwa anaachiwa huru kwa kweli inaumiza sana,"amesema Mkurugenzi Dakawa

Aidha ameishauri mahakama kuwafunga watuhumiwa wanaokutwa na hatia ili wawe mfano katika jamii kwani vitendo hivyo vinawanyima raha wanan-

chi hasa wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

Akiongea kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondoa Mohamed Kiberenge amesema halmashauri itaona jinsi ya kukazia suala la kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia katika sheria ndogo za Halmashauri na kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi ili Mji wa Kondoa uwe na nidhamu pamoja na amani na utulivu.

"Nashauri vijana wajengewe uwezo kwa kupewa elimu ya ujasiriamali na michezo ili kuwaepusha na mawazo ya kufanya mambo yanayosababisha wao kufanya ukatili kwakuwa tupo katika taifa linaloheshimu utu wa mtu,"amesema Mhe. Kiberenge.

Wakichangia mada waalikwa mbalimbali katika mdahalo huo walishauri vyombo vya usalama kuendelea kuwashughulikia watuhumiwa wa kesi za ukatili,

viongozi wa dini kuendelea kutoa elimu ya dini kwa waumini wao na kuendelea na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwakutumia vyombo vya habari.

Mdahalo wa kupinga ukatili wa kijinsia umefanyika katika Halmashauri ya Mji Kondoa ikiwa ni maadhimisho ya kilele cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na umehudhuriwa na waheshimiwa madiwani, viongozi wa dini, wakuu wa Idara, wanafunzi, wananchi na wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali ambapo kauli mbiu mwaka huu ni tupinge ukatili wa kijinsia mabadiliko yanaanza na mimi.



Mkurugenzi Kondoza Mji ateta na Walimu Wakuu

Walimu wakuu wa Halmashauri ya Mji Kondoza wameaswa kufanya kazi kwa ubunifu, nidhamu, kutambua mamlaka zao na zinazowaongoza ikiwa ni pamoja na kufuatilia masuala ya kitaaluma kwa wanafunzi na walimu ili kuongeza ufaulu katika shule wanazoziongoza.

Ushauri huo umetolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoza Msoleni Dakawa wakati wa ufunguzi wa kikao cha Walimu Wakuu kilichofanyika katika ukumbi wa Kituo Cha Walimu Kondoza Mjini hivi karibuni.

"Nikiwaangalia wote hapa mna uwezo mkubwa sana na mnaweza kufanya makubwa katika shule zetu ila hamjaamua kujituma na sijui kwanini mnafanya hivyo sababu ninachojua mimi wakati wa kujituma kwenu ni sasa wakati mkiwa viongozi na si mkishatolewa," amesema Dakawa

Aidha ameongeza kuwasihikuendelea kufanya kazi kwa nguvu zote na kuacha alama wamefika hapo

kwa kuwa kazi wanazofanya zina mkuo wa Mungu sababu wanawahudumia watoto ambao wanapaswa kuwakumbuka kwa mazuri wanayowafanyia na si mabaya.

"Nawaambieni hawa maafisa elimu wametokea hukohuko kwenye ualimu hakuna aliyezali-



Mkurugenzi Kondoza Mji Msoleni Dakawa (aliyesimama pichani) akihutubia walimu wakuu wakati wa ufunguzi wa kikao cha walimu kilichofanyika katika kituo cha walimu Kondoza

zote kunalipa," amesisitiza Mkurugenzi Dakawa

Hata hivyo amewataka kufanya kazi kwa kuunganisha walimu wanaoawaongoza na kuacha tabia za kuwa miungu watu na ikitokea Mwalimu kakosea wamwite na kumueleza mapungufu yake ili asirudie makosa kin-yume na kufanya hivyo watatengeneza makundi na kuleta migogoro katika taasisi.

"Baadhi yenu mnaletewa miradi mnashindwa kuisimamia hii siyo sawa kwa kuwa serikali inatoa fedha nyingi, lakini mkumbuke nyie mna posho za madaraka hivyo zitumieni kwa kufanya kazi kwa kujituma lengo ni moja kuhakikisha Halmashauri yetu inafaulisha wanafunzi wote," amesema Mkurugenzi Dakawa

Aidha ameendelea kuwataka kifanyakazi kwa kushirikiana na viongozi wa mitaa ili kuhakikisha

wanakamilisha utengenezaji wa madawati ili kuhakikisha hadi jituma kufanya ifikapo Januari 11 hakuna mwakazi na nidhamu nafunzi anayekaa chini.

kwa kuwa Akiongea awali Afisa Elimu kufanya kazi Msingi Halmashauri ya Mji Kondoza kwa bidii siku kwa Mwalimu Hassan Mtamba

Baadhi ya wakuu wa Shule za Msingi Halmashauri ya Mji Kondoza wakimsikiliza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Msoleni Dakawa (Hayupo pichani) wakati wa kikao cha pamoja na Idara ya Elimu Msingi



Waliovamia Kondoza Girls watakiwa kuondoka



Mwanasheria wa Halmashauri ya Mji Kondoza Shabani Sued akiongea na mmoja wa wananchi waliovamia maeneo ya Shule ya wasichana Kondoza wakati wa uhakiki wa mipaka ya maeneo hayo uhakiki uliofanywa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mkurugenzi, menejimenti na walimu wa Shule hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoza Msoleni Dakawa amewataka mwananchi wote waliovamia na kupewa notisi katika maeneo yanayomilikiwa na Shule ya Wasichana Kondoza kuondoka mara moja kabla ya kufika mwisho wa notisi hizo.

Ameyasema hayo alipotembelea mipaka ya maeneo hayo ili kujiridhisha na mipaka ya shule hiyo ambapo alikutana na wananchi waliovamia maeneo hayo wakiendelea na shughuli za kilimo.

"Nawashauri msijaribu kuen-delea na shughuli za kilimo kati-ka maeneo haya ya shule na kama kuna mtu anakodisha msikubali hakuna mtu anayemiliki maeneo haya zaidi ya shule leo tumekagua maeneo haya kujiridhisha mipaka tumeona beacons zote zipo hivyo msivuke tena ndani ya eneo hilo", amesema Mkurugenzi Dakawa

Aidha amesikitishwa na baadhi ya wavamizi kung'oa na kuvunja beacons na kuziweka maeneo mengine kwa lengo la kupindisha ukweli na kuagiza wataalam

wa Idara ya ardhi kwenda kupi-ma maeneo ambayo beacons zimetolewa ili kuweka kumbukumbu sahihi za eneo hilo. Katika ukaguzi huo Mkurugenzi aliongozana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondoza Mhe. Mohamed Kiberenge, wataalam toka idara mbalimbali za Halmashauri na walimu wa Shule ya Wasichana Kondoza ambapo eneo la ukubwa wa hekta 78 limevamiwa na wananchi na Halmashauri imewapa notisi ya siku 21 watu hao kuondoka katika maeneo hayo.

Wasimamizi wa vituo vya kupigia kura wafundwa



Wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa vituo vya kupigia kura wakila kiapo kilichotolewa na Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Kondoa Msoleni Dakawa (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa semina ya siku mbili kwa ajili ya uchaguzi mkuu katika chuo cha uwalimu Bustani.

Msimamizi wa Uchaguzi jimbo la Kondoa Mjini Msoleni Dakawa amewataka wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa vituo vya kupigia kura wakati wa uchaguzi mkuu kuzingatia maelekezo watakayopewa ili kuuvusha salama uchaguzi jimbo la Kondoa Mjini.

Kauli hiyo ameitoa wakati aki fungua semina ya siku mbili ya wasimamizi hao inayofanyika katika ukumbi wa Chuo Cha Ualimu Bustani Kondoa Mjini.

"Kila mtu anajua kwanini ameteuliwa na mkumbuke mliomba mlikuwa wengi ila nyie wachache mmeaminiwa kuwa mtalivusha salama taifa katika zoezi linalokuja mbele yenu na mjue kwasasa macho na masikio ya watu wote yapo majimboni msitu-

angushe,"amesema Dakawa.

Aidha amewakumbusha kuwa uchaguzi upo wa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali hivyo wakavizingatie kwani kwenda kinyume na hivyo watawajibika kwa mujibu wa sheria jambo ambalo si zuri kwao.

"Sitarajii kukutana na migogoro na mitafaruku kwenye vituo vya kupigia kura zaidi mkashirikiane kama timu moja kwani kila mmoja katika kituo ana majukumu yake,"amesisitiza Dakawa

Hata hivyo amewasihi wasimamizi hao kuepuka kuleta itikadi za vyama vyao kwa kuwa wameshakula kiapo cha kujitoa uanachama na wakumbuke kuwa wapo pale kama watumishi wa tume na serikali na si wanasiasa.

"Mkazingatie muda wa kufika kituoni, kituo kinafunguliwa saa 1:00 asubuhi na si muda wa wewe kufika kituoni na ujue kuchelewa kwako ni kuwakwamisha wananchi, na kubwa mkamtangulize Mungu katika kazi hii ili mmalize salama," amesema Dakawa

Akiongea kwa niaba ya wasimamizi wengine Zainabu Shabani amewasihi washiriki wengine kwenda kuwa waaminifu katika kukamilisha zoezi hilo

**“KURA YAKO
SAUTI YAKO
EWE MWANANCHI
WA KONDOA
NENDA UKAPIGE
KURA”.**

Hachwi watakiwa kuacha tofauti ujenzi wa Zahanati.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Hassan Kiseto akiongea na wananchi wa Mtaa wa Hachwi katika mkutano wa hadhara kwa ajili ya kuweka mikakati ya ujenzi wa Zahanati ya Mtaa huo baada ya serikali kutoa shilingi milioni 50 katika mtaa huo.



Wananchi wa mtaa wa Hachwi katika Halmashauri ya Mji Kondoa wametakiwa kuacha tofauti zao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwani kwa kufanya hivyo wanachelewesha upatikanaji wa huduma muhimu kwa wananchi.

Hayo yamesemwa na Kaimu Mkurugenzi Hassan Kiseto wakati wa mkutano wa wananchi kuhusu ujenzi wa Zahanati ya Mtaa huo uliofanyika katika ofisi za mtaa wa Hachwi hivi karibuni.

"Mradi huu ulitakiwa uwe umeshaanza toka kitambo fedha zipo kwenye akaunti shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hapa lakini ujenzi haujaanza kwa kuwa mnavutana eneo la kujenga zahanati siyo sawa tunataka kuona kazi inaanza ili lengo la serikali la kuona huduma zinasogezwa karibu kwa wananchi linatimia," amesema Kiseto.

Aidha ameongeza kuwa kwa kuwa wananchi wote wanavutana juu ya eneo la kujenga zahanati ni wazi kuwa wote wanahamu ya kupata maendeleo na kuwaagiza wananchi

hao kujenga jengo la Zahanati ilipokuwa zahanati ya awali na wengine kujenga nyumba mbili za watumishi kwa ajili ya kituo cha afya katika eneo lilipo shamba la mtaa.

Akiongea awali diwani wa kata ya Kolo Mhe. Idd Ng'ungu amesema wananchi wa mtaa huo wananeema ya kupata miradi kwani hadi sasa wamepewa miradi minne muhimu kwa mwananchi hao ambayo ni usambazaji wa maji, ujenzi wa madarasa na nyumba ya mwalimu shule shikizi ya Kotumo, ujenzi wa Zahanati ya Hachwi na ufunguzi wa barabara.

Akielezea tatizo lililocheleweshwa kuanza kwa mradi huo Mtendaji wa Mtaa wa Hachwi Judith Mkumbwa amesema mvutano ulianza baada ya wananchi ya baadhi ya wananchi kutaka zahanati ijengwe eneo la shamba la wananchi na kupelekea wananchi kuanza kusita kuchangia mchango wa shilingi elfu 10 wali-okubaliana.

Kwa upande wao akina mama na baadhi ya wananchi wameomba Zahanati ijengwe ilipokuwa zahanati ya awali kwa lengo la kuhakiki-

sha wananchi wa maeneo yote ya mtaa wa Hachwi wanafika kwa urahisi zahanati kwa ajili ya kupata huduma za afya.

"Wakina mama sisi ndio tunaoteseka sana katika zahanati yetu hii ya awali tumekuwa tukipata huduma ya mama na mtoto na hapa ni karibu kwa kila mtu lakini kwasasa inatulazimu kukodisha pikipiki hadi hospitali ya wilaya lakini tumeletewa fedha za kujenga zahanati hapa karibu alafu eti tunataka kuipeleka kule mbali tena tutarudisha gharama zilezile za kukodisha pikipiki nashauri mtusaidie ijengwe hapa-hapa ili kila mtu apate huduma kwa ukaribu," amesema mmoja wa akina mama.

Mkutano wa uhamasishaji ujenzi wa zahanati ya Hachwi umekuja kwa lengo la kutatua changamoto ya mvutano uliokuwepo awali wa kuchagua eneo la kujenga Zahanati baada ya serikali kutoa shilingi milioni 50 ambapo wataalam mbalimbali wa halmashauri walihudhuria wakiwemo Mwanasheria, Afisa Maendeleo ya Jamii, Kaimu Afisa Mipango, Kaimu Afisa Utumishi, Kaimu Mhandisi, Kaimu Mganga Mkuu na Kaimu Afisa Elimu.

Wasiohudhuria mkutano wa wananchi Unkuku kutozwa faini



Afisa Tarafa Kondoaa Mjini Ally Mbena (aliyesimama pichani) akihutubia wananchi wa mtaa wa Unkuku

Wananchi wa Mtaa wa Unkuku kata ya Kilimani ambao hawakuhudhuria mkutano wa wananchi wa uhamasishaji wa ujenzi wa madarasa Shule ya sekondari Bicha wamepewa wiki moja kulipa faini ya shilingi elfu mbili ili iwe fundisho kwa wakati mwingine.

Hayo yamesemwa na Afisa Tarafa Kondoaa Mjini Ally Mbena wakati wa mkutano wa wananchi wa mtaa huo uliofanyika katika uwanja wa ofisi ya Mtaa na kuhudhuriwa na wananchi wachache tofauti na idadi ya wakazi wa mtaa huo.

"Nimemuuliza Mwenyekiti mbona wananchi wachache leo tofauti na mkutano wa awali lakini kaniambia sababu ule ni mkutano wa masuala ya TASAF ndio maana wananchi walikuja wengi siyo sawa hii tusibague mikutano yatayozungumzwa hapa yanahitaji maamuzi ya pamo-

ja," amesema Mbena

Hata hivyo aliongeza kuwa jambo lililopo kwasasa ni ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari Bicha hivyo ni wajibu wa wananchi wote kuchangia ili kuhakikisha ujenzi unakamilika kwa wakati kwani hadi sasa wapo nje ya wakati lengo ni kuhakikisha watoto wote waliofaulu wanaenda shuleni.

"Nawasihi sana ndugu zangu tuendelee pia kuwaandalia watoto wetu mahitaji muhimu ili shule zikifunguliwa waende shuleni kwani taarifa za ufaulu si za ghafla matokeo yamebandikwa wilayani lakini pia yatabandikwa ofisi ya Mtaa ili kila mtu aone mwanaye anaenda shule gani lakini nitumie fursa hii pia kuwakumbusha kuwaandikisha watoto wa awali na darasa la kwanza ili wapate haki yao ya msingi," amesisitiza Mbena.

Naye mwakilishi wa Mkurugenzi Mwalimu Selina Fundi amesema kuwa ujenzi huo wa madarasa katika Shule ya Bicha umekuja kutokana na kuongezeka kwa ufaulu kwa mwaka huu ambapo jumla ya wanafunzi 279 wamechaguliwa kujiunga na shule hiyo hivyo mahitaji ni vyumba 6 na shuleni hapo kuna madarasa manne ndio maana umetokea upungufu wa vyumba viwili ambavyo tayari vimeanza kujengwa kwa kutumia mapato ya ndani.

"Maendeleo yanaletwa na sisi wananchi hivyo tukitoe kwa hali na mali kuhakikisha madarasa yanaisha lakini tutashirikiana na Halmashauri kujenga madarasa na pia tuna upungufu wa viti na meza 323 hivyo tutahitajika kujitoa pia kwa hilo na tumeshaanza upasuaji wa mbao ili kukabiliana na upungufu ili watoto wasome katika mazingira mazuri," amesema Mwalimu Selina.



Watumishi na wananchi wakifuatilia kongamano la kupinga ukatili wa kijinsia lililofanyika katika ukumbi wa Kondoa Irangi

Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Mji Kondoa imejipanga kusimamia kesi za ukatili wa kijinsia walizofanyiwa wakazi wa Halmashauri hiyo ili kuhakikisha haki inatendeka kwa waliofanya vitendo hivyo.

Hayo yamesemwa na Bi. Irene Mosha Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wakati wa utoaji elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Bolisa na wananchi wa mtaa wa Msui hivi karibuni.

"Naomba wananchi wote ambao mna kesi za ukatili wa kijinsia ambazo hazijashughulikiwa mzirodheshe na kuziwasilisha ofisini ili nizifikishe polisi kwa ajili ya msaada zaidi lengo ni kukomesha vitendo hivi katika jamii yetu," amesema Irene

Aidha aliwasihi wanafunzi kutoa taarifa kwa walimu wao wakuu au uongozi wa mtaa mara wanapo-

fanyiwa vitendo vya ukatili ili wahuusika wachukuliwe hatua kwani huwasababishia maumivu wanafunzi hao na kuwarudisha nyuma



Afisa Maendeleo ya Jamii Bi. Irene Mosha akizungumza na wananchi wa mtaa wa Msui (kushoto pichani) pamoja na wanafunzi wa Shule ya Msingi Bolisa (pichani hawapo) wakati wa utoaji wa elimu ya ukatili wa kijinsia.

kitaaluma.

Naye Mwalimu Mkuu Msaidizi katika Shule ya Msingi Bolisa Bi. Victoria Mwidunda amesema kati-

ka shule yake mwanafunzi mmoja alipigwa na mama yake wa kambo na kupata majeraha ambapo walisaaidiana na kuhakikisha mtuhumiwa anakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria na kwasasa anatumikia kifungo gerezani.

Hata hivyo mmoja wa wanafunzi ameshukuru kwa kupatiwa elimu hiyo na kuahidi kutoa elimu kwa watu wengine na kutoa taarifa mara tu watapofanyiwa ukatili ili kukomesha vitendo hivyo.

Utoaji elimu ya ukatili wa kijinsia umefanyika ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ambapo Halmashauri imeshirikiana na wadau CCT ambao wametoa elimu na kugawa vipeperushi katika kata ya Kingale na Bolisa na mwaka huu kauli mbiu inasema Tupinge ukatili wa kijinsia: Mabadiliko yanaanza na wewe"

MATUKIO MBALIMBALI OKTOBA-DISEMBA 2020



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota (wa tano kutoka kushoto) akiwa na waheshimiwa madiwani baada ya uzinduzi wa baraza la Madiwani la 2020-2025



Maji ya Shamba Shule ya Msingi

Muonekano wa madarasa mapya katika Shule ya Msingi Maji ya Shamba yakiwa yamekamili baada ya kupokea fedha kutoka serikali kuu kupitia mradi wa EP4R.



'Ula Sekondari

Muonekano wa madarasa mapya katika Shule ya Sekondari Ula yakiwa yamekamili baada ya kupokea fedha kutoka serikali kuu kupitia mradi wa EP4R.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Iboni akimwandikisha mwanafunzi wa darasa la kwanza shuleni hapo wakati wa zoezi la uandikishaji wanafunzi wa awali na darasa la kwanza kwa mwaka 2021.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondo (kushoto) akiwaonyesha jinsi ya kushona nguo wanafunzi wa Shule ya Ufundi Kilimani na (kulia) mwanafunzi wa Shule ya Ufundi Kilimani akishona nguo shuleni hapo.

